

SWALI: Nini maana ya Kumbukumbu 25:11

*Kumbukumbu 25:11 “Washindanapo waume wao kwa wao,
akakaribia mke wa mmojawapo, ili kumwokoa mumewe katika
mkono wa ampigaye, yule mke akatoa mkono wake, na kumkamata
tupu yake; 12 umkate ule mkono wake, lisiwe na huruma jicho
lako”*

JIBU: Bwana asifiwe, Haya ni mafundisho maalumu wayahusuyo wanandoaa. Lakini pia kanisa la Kristo.

Kama ukiutafakari mstari huu, utaona picha ya mwanamke mwenye huruma, ambaye, ameona mume wake, anapigana na adui yake, na pengine alikuwa anakaribia kushindwa. Hivyo kwasababu ya upendo wake kwa mumewe, akaamua kwenda kumwokoa. Lakini tunaona njia aliyoitumia badala imletee alilolitarajia, ikamletea matatizo yeye mwenyewe.

Kwasababu gani? Kwasababu alikwenda kugusa sehemu zake za siri, Na hiyo ikawa kosa kwake, lililostahili adhabu ya kukatwa mkono. Laiti kama angemkamata mahali pengine labda tuseme mguuni, au

penginepo, ni wazi kuwa kusingekuwa na adhabu yoyote au adhabu iliyo kali namna ile.

Ni kufunua nini?

Ni mipaka ya mwanamke awapo ndani ya ndoa yake. Fikiria hata kwa adui ya mume wake huyu mwanamke, hukupaswa kuvuka mipaka ya kindoa, si zaidi kama angefanya hivyo kwa rafiki wa karibu wa mume wake ndio ingekuwa kosa kubwa kabisaa?. Leo hii kumekuwa na migogoro mingi ndani ya ndoa, na ukitazama utagundua tabia ya wanawake kutojiwekea mipaka yao, wakutanapo na wanaume wengine wa nje.

Kwamfano mwanamke yupo kazini. Halafu Boss wake/ mfanyakazi mwenzake anazungumza mazungumzo ya mizaha, ya kizinzi, utaona na ye ye analiridhia hilo, au kulifurahia au anaona ni kawaida tu. Anashindwa kujiwekea mipaka, Anaipoteza nidhamu yake, anaruhusu mazoea yaliyopitiliza ambayo hayampasi mtu kama ye ye kuwa nayo. Sasa hiyo ni hatari kubwa.

Wewe kama mwanamke unapaswa ujiwekee mipaka ya hali ya juu. Uki ona migororo inaendelea baina ya wanaume, jiwekee mipaka ya kitabia na kimwenendo. Uwe salama, ili mkono wako usifike kusikostahili. Uvaaji wako, usemi wako, uwe kama mtu aliye kwenye

“KIFUNGO” cha ndoa. Watu wakuheshimu, wenye mizaha wakuonapo wakae kimya. Usiruhusu kabisa mazungumzo yako na mtu mwingine yafike kwenye maeneo ya sirini, iwe kwenye simu, ofisini, njiani, shuleni, mtaani, nyumbani, au popote pale. Weka MLANGO mkubwa wenye makomeo ya chuma . Mazungumzo hayo yawe na mume wako tu, na sio mwingine yoyote.

Halikadhalika inatupa na picha ya rohoni pia. Sisi kama kanisa ni lazima tufahamu kuwa wote ni “WAKE” wa Bwana wetu Yesu Kristo. Na hivyo anataka tuwe na tahadhari tuendapo kumuhubiri yeye kwa watu wa nje, tujichunge tusijaribiwe wenyewe, kwa vitendo vyao. Kwasababu itatugharimu kinyume chake.

Tukutanapo na wazinzi kuwahubiria, tusivutwe kwenye uzinzi wako, tukutanapo wa watukanaji, tusirudishe matusi, tukutanapo na wenye fedha, tusigeuzwe injili yetu. Bali tubaki kwenye mipaka yetu ile ile.

Wagalatia 6:1 Ndugu zangu, mtu akighafilika katika kosa lo lote, ninyi mlion wa Roho mrejezeni upya mtu kama huyo kwa roho ya upole, ukijiangalia nafsi yako usije ukajaribiwa wewe mwenyewe.

Bwana akubariki.

Pia kwa kupokea mafundisho ya kila siku kwa njia ya WHATSAPP, jiunge na channel yetu kwa kubofya link

hii >> <https://whatsapp.com/channel/0029VaBVhuA3WHTbKoz8jx>

10

Tafadhali shea na wengine ujumbe huu;

Pia Kwa maombezi/ Ushauri/ Maswali/ Whatsapp:

Tuandikie katika BOXI la Maoni hapo chini au

Piga namba hizi: +255789001312 au +255693036618

Mafundisho mengine:

**Nini maana ya Mithali 16:30 Afumbaye macho, kusudi lake ni
kuwaza yaliyopotoka;**

**Maana ya Mithali 29:21 “Amtundaiaye mtumwa wake tangu
utoto, Mwisha wake atakuwa ni mwanawe”**

Kula uzao wa tumbo lako maana yake nini? (Kumbukumbu 28:53)

Ielewe vema Kumbukumbu 25:11,inamaana gani.

MISTARI YA BIBLIA KUHUSU NDOA.

USIONDOE ALAMA YA MPAKA ILIYOWEKWA NA MABABA.

**Kwanini kuwe na kitabu Cha kumbukumbu la Torati na kwanini
kiitwe vile?**

Rudi nyumbani

Share on:

WhatsApp

[Print this post](#)